



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE



*Mwalimu mkoani Moroqoro akifundisha wanafunzi kusoma kwa kutamka herufi*

*Picha: Rachel Chilton/USAID*

## TANZANIA

### JIFUNZE UELEWE

*Jifunze Uelewe ni mradi wa miaka minne ambao unalenga kuendeleza uboreshaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi wote katika elimu ya awali na msingi.*

*Tanzania imeshuhudia ukuaji wa kasi ya upatikanaji wa elimu ya msingi, lakini matokeo na ubora wa elimu na ufundishaji yanabaki kuwa chini kuliko nchi zingine. Tangu kuanzishwa kwa elimu ya bila malipo ya ada, idadi ya walimu imeshindwa kuendana na ongezeko la mahitaji ya wanafunzi, hasa kutoka kwa watoto wenye ulemavu. Jitihada za jifunze Uelewe zinatokana na kuongezeka kwa matokeo ya kujifunza, kusoma na kuhesabu kwa wanafunzi wote.*

Malengo ya *Jifunze Uelewe* ni:

1. Kuboresha ujuzi wa walimu wa kusoma na kuandika, kuhesabu na mafunzo ya kijamii na kihisia.
2. Kuimarisha uwezo wa ndani na kikanda katika kuendeleza na kuongeza ufundishaji ulioboreshwa.
3. Kuongeza usaidizi wa jamii kwenye elimu salama na jumuishi ndani na nje ya shule.

**BAJETI**

Dola za Marekani 38.6 Milioni

**MUDA WA MRADI**

April 2021 - Oktoba 2025

**MAENEO MRADI  
UTAKAPOTEKELEZWA**

- Morogoro
- Iringa
- Mtwara
- Ruvuma
- Zanzibar

**MTEKELEZAJI**RTI International <https://rti.org/>**WASHIRIKA**

Government of Tanzania

**MAWASILIANO YA USAID**

Laura Kikuli

Project Management Specialist - Education

T+255 22 2294490 ext 4881 | M +255 715

046 832

Fax: +255 22 2294421 |

**MAWASILIANO YA MSHIRIKA****Sylvester Isuja, MA**

Chief of Party,

RTI International [www.rti.org](http://www.rti.org)

+255 787 202280 or +255 757 202283

[Sisuja@jifunzeuelewe.rti.org](mailto:Sisuja@jifunzeuelewe.rti.org)

Skype: Sylvester Isuja

**KWA TAARIFA ZAIDI**Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)

Facebook: USAIDTanzania

Twitter: @USAIDTanzania

**AFUA ZA MRADI**

Afua za Jifunze Uelewe zimeundwa kulingana na vipaumbele vya Mkakati wa Kitaifa wa Serikali ya Tanzania wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu Jumuishi. Afua hizi ni:

- Kufanya kazi na walimu ili kutumia kwa ufanisi zaidi nyenzo za kufundisha na kujifunzia hesabu darasani.
- Kutoa mafunzo kwa walimu, walimu wakuu na maafisa wa elimu wa kata kuhusu mbinu za kusoma na kuandika zinazo tegemea fonetiki.
- Kubainisha udhaifu na vikwazo katika jumuiya za shule ambavyo vinazuia wanafunzi kupata ufasaha wa kusoma na kuhesabu.
- Kutoa vifaa vya shule vilivyo jumuishwa na salama na nyenzo za kusaidia kusoma na kuhesabu.
- Kutoa mafunzo kwa wazazi na walimu katika mikakati ya kijamii na kitabia ili kusaidia jumuiya ya kujifunza ilio salama na jumuishi.
- Kushirikisha jumuiya za shule katika uanzishaji wa shughuli za kusoma nje ya shule.

**MATOKEO YANAYOTARAJIWA**

Mwisho mwa mradi huu, matokeo yafuatayo yanatarajiwa:

- Kuboresha stadi za kusoma na kuhesabu kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la nne
- Uboreshaji wa muundo wa shule katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Mtwara, Ruvuma na visiwani Zanzibar.